**MPANGO WA MUNGU WA MAISHA YA MWANADAMU**

Mungu ana mpango wa maisha ya mwanadamu. Mapango huu wake ulianza kabla ya dunia kuumbwa.
Tazama Zaburi 11:1

MSIFUNI BWANA
Nitamshukuru bwana kwa moyo wangu wote,
Barazani pa wanyofu wa moyo na katika mkutano.
Matendo ya bwana ni makuu,
Yafikiriwa sana na wapendezwao nayo.
Kazi yake ni heshima na adhama.
Na haki yake yakaa milele.
Amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu,
Bwana ni mwenye fadhili na rehema.
Amewapa wamchao chakula,
Atalikumbuka agano lake milele.
Amewjulisha watu wake uwezo wa matendo yake.
Kwa kuwapa uridhi wa mataifa.
Matendo ya mikono yake ni kweli na hukumu,
Maagizo yake yote ni amini,
Yamedhibitika milele na milele,
Yamefanywa katika ukweli na adili.
Amewapelekea watu wake ukombozi,
Ameamuru agano lake liwe la milele,
Jina lake ni takatifu la kuogopwa.
Kumcha Bwana ndicho chanzo cha hekima,
Wote wafanyao hayo wana akili njema.
Sifa zake zakaa milele.

Kila wakati tunapomhimiza mtu kumtazama Mungu nasi huwa tunamtazama Mungu katika hali zetu, kwa sababu Mungu ametufanya mabalozi wake na tunashiriki upendo wake na ulimwengu. Unaposhiriki katika mpango wa Mungu katika maisha yako, unashirikishwa katika neno la Mungu lipatikanalo katika Isaiya 52:7-12.

Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima,
Miguu yake aletaye habari njema,
Yeye aitangazaye amani,
Aletaye habari njema ya mambo mema,
Yeye autangazaye wokovu,
Auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki!
Sauti ya walinzi wako!
Wanapasa sauti zao wanaimba pamoja,
Maana wataona jicho kwa jicho,
Jinsi Bwana arejeavyo Sayuni.
Pigeni kelele za furaha, imbeni pamoja,
Enyi pahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa,

Kwa kuwa Bwana amewafariji watu wake,
Ameukomboa Yerusalemu
Bwana ameweka wazi mkono wake mtakatifu.

Machoni pa mataifa yote,
Na ncha zote za dunia .
Zitauona wokovu wa Mungu wetu.

Neno la Mungu linatuahidileo kuwa ametupatia uzima katika Bwana Yesu Kristo.Ni wazuri namna gani wale waletao habari njema ya furaha kuu!
Malaika walitangaza kuzaliwa kwa Yesu Kristo katika ulimwengu huu Waliimba
“Leo tunatangaza furaha kuu,kwa kuwa leo Mwokozi amezaliwa kwenu,Kristo Bwana”(Luka 2:10,110)
Kwa sababu Yesu alidhihirika,malaika mbinguni walifurahi kwa kuwa Mungu alikuja kuwafungua watu wake.Walifurahia mpango wa Bwana wa uzima akienenda kwa niaba ya watu wake nao wakaufurahia mpango huo.
HISTORIA YA BINADAMU
Na tuutazame mpango wa Mungu tukianza na Adamu . Adamu aliumbwa akifanana na Mungu sana, akiwa hana dosari yoyote na mtakatifu. Alikuwa na ushirika mkamilifu na Mungu, lakini akachagua kuwa muasi. Alimwondokea Mungu bila matarajio ya kurudi, akiwa amepotea na kutengwa milele. Hata hivyo Bwana wakati huo huo aliufanya mpango wa kuwaokoa wanadamu na kuwarejesha kwake tena. Mpango wake ulianza na Adamu, binadamu wa kwanza na umekuwa ukiendelea kila wakati.

Katika historia yote Mungu amekuwa akiwaita watu lakini wamekuwa wakimuasi na kufuata njia zao.

Wakati wa Nuhu, Mungu alifikiria kuwaangamiza watu na kuanza tena kwa sababu hakukuwa na yeyote aliyemfuata Bwana ispokuwa Nuhu. Mungu alimwagiza Nuhu kujenga safina kwa kuwa Mungu wakati huo alitaka kuiangamiza dunia kwa maji ya gharika. Nuhu na jamii yake waliokoka pamoja na wawili wawili wa kila mnyama. Bwana atakuwa tena na alichokiumba akitarajia kuwa na watu ambao watakubali na kufurahia (kutoka mioyo yao) upendo wake.

Wakati ukaendelea na Bwana akawastawisha watu  ambao amewatenga kumpenda, kumheshimu na kumsifu. Alimwahidi Ibrahimu kuwa kutokana na mbegu yake taifa kubwa litazaliwa na litatawala  mataifa mengine yote. Ahadi hii ilifanywa kwa mtu mwenye umri wa miaka 100 na mkewe alikuwa tasa. Alimwamini Mungu kiliko jinsi hali zilivyokuwa.

Mungu kwa kimiujiza alimpatia Ibrahimu mwana wa kiume, Isaka. Jina hili linamaanisha ‘kicheko’ kwa maana Sara na Ibrahimu walicheka kwanza walipopewa ahadi hii. Wakati mwingi hekima ya Mungu ni ujinga kwa mwanadamu. Isaka alikuwa na mwana Yakobo na ahadi hii ikaendelea. Baadaye Mungu akabadilisha jina la Yakobo likwa “Israeli”.

Ni kutokana na Yakobo taifa hili kubwa la Israeli likaanza. Walienda utumwani Misri lakini Mungu akaendelea kuwapanua.

Mungu aliwaita viongozi wa watu wake kufuata njia alizotaka wafuate. Musa alikuwa mmoja wa viongozi hao wakati wana wa Israeli walikuwa utumwani kama watumwa huko Misiri, Bwana alikuwa na mpango wa kuwakomboa. Tunajua yaliyofanyika kutoka kitabu cha Kutoka Mungu alijidhihirisha mwenyewe kupitia Musa wakati alienda mbele ya Farao. Mungu alifanya ishara na maajabu (miujiza) iliyowafanya watu kupata ukombozi.

Uhuru wao uliannza na Pasaka. Usiku huo watu walichukua wana- kondoo ambao hawakuwa na dosari kama jamaa zao zilivyokuwa. Walichukuwa damu ya mwana kondoo na kuipaka kwenye

kizingiti cha juu na miimo miwili ya mlango kwa maana malaika wa kifo hangeua yeyote kwenye nyumba iliyopakwa damu.

Baada ya Pasaka, Bwana aliwaita watu wake pamoja na kuhama misiri. Kwa kweli Baraka za Mungu zilikuwa juu yao kwa wingi mpaka Wamisri walifurahia kuondoka kwao na kuwatajirisha kwa kila aina ya utajiri. ( Mungu alikuwa akiwabariki watu wake).
Mungu aliwaokoa na ishara kuu na maajabu yaliwafuat. Bahari iliiitenga na kwa kufanya hivi Mungu akawakomboa watu wake kutoka misri milele. Aliendelea kuwashughulikia na kuwakidhia mahitaji yao kwa njia kuu mchana na usiku ndani ya mfano wa nguzo na mchana ndani ya wingu mfano wa nguzo na watu walifurahia Mungu wao.

Mungu alianza kuwainua juu ya mataifa yote Mataifa yote yaliona kuwa Mungu wa Israeli ni Mungu mwenye nguvu na mkuu na hakuna mwingine kama yeye.

Hata hivyo kizazi cha kwanza cha Waisreali kiliasi na kikakosa kumtii Mungu. Walikosa shukrani kwa Mungu, wakawa wagumu na waasi. Walifia jangwani kwa sababu hawakuamini ahadi ya Mungu. Jinsi wana wa Israeli walivyokuwa wakitanga jangwani, Mungu aliwafanyia sheria zake kwake ndiposa waweze kufahamu njia zake na kufanikiwa. Sheria zake zilitolewa katika mlima Sinai ili watu waweze kujua mapenzi yake yalivyo ndiposa wayatii na kubarikiwa. Huu ulikuwa mpango wa Mungu. Wakikosa kutii mapenzi yake walikosa Baraka zake.
Kizazi kilichofuata kilijimuisha wale walioingia nchi ya Kanani, nchi ya ahadi ambayo Mungu aliwatengea watu wake kutoka mwanzo. Waliishi katika nchi hiyo na kumfurahia Mungu wao. Walishinda maadui wao wote kwa sababu Mungu alikuwa nao na aliendelea kutembea kimiujiza ili kuwastawisha watu wake. Hata hivyo mara kwa mara walimuasi Mungu wakitaka kuishi kivyao na kufuata njia zao.

Mungu aliwainua viongozi ambao waliwafanya watu wamwone kuwa Mungu pekee yake na waiache miungu mingine yote waliyokuwa nayo. Viongozi hawa walijulikana kama waamuzi na manabii.

Manabii waliendelea kuwaonyesha watu kuwa wanamhitaji Mungu na wanatakiwa kumtegemea Mungu (na njia zake) ikiwa wataendelea kuwa na uzima.

MJO WA AHADI
Katika Isaiya 52:13 tunaona ahadi iliyotabiri kile Mungu alitaka kiwajie watu wake ili Mungu awakomboe mara moja ya kutosha. “Tazama mtumishi wangu atatenda kwa busara, atatukuzwa na kuinuliwa juu sana. Yeye ndiye angeteseka kwa niaba ya watu ili awakomboe.

Kama vile wengi walivyokustaajabia,(uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya mwanadamu)ndivyo atakavyowashtusha mataifa mengi, wafalme watamfumbia vinywa vyao maana mambo wasiyoambiwa watayaona na mambo wasiyoyasikia watayafahamu (Isaiya 52:14-15)
Ahadi ya Mungu kwa niaba ya watu wake ilitabiriwa karne nyingi kabla yake kutimika.

Ni nani aliyesadiki habari mliyoileta?
Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani?
Maana alikuwa mbele zake kama mche mwororo,
Na kama mzizi katika nchi kavu:
Yeye hana umbo wala uzuri;
Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.
Alidharauliwa na kukataliwa na watu;

Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko;
Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao,
Alidharauliwa wala hamkumhesabu kuwa kitu.
Hakika anayechukua masikitiko yetu,
Amejitwika huzuni zetu;
Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa,
Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu,
Alichumbuliwa kwa maovu yetu,
Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake,
Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. (Isaiya 53:1-5)

Hii ilikuwa ahadi ya Mungu, kutabiri kuwa Yesu angekuja kuwakomboa watu wake. Akinena karne nyingi baadaye, Yesu alisema, “Mwivi haji ili aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nilikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele. (Yohana 10:10). Shetani ndiye alisababisha Adamu na Hawa kuljaribiwa na kumwondokea Mungu hata ikiwa walijichagulia kufanya hivyo,Mungu alitengeneza njia ya mwanadamu kumrudia tena. Lazima angetembea kwa niaba ya mwanadamu.

## SIFA ZA YESU

Yesu alisema, “Mimi ndimi njia, na ukweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi”(Yohana 14:6) pia alisema,”Mimi nilikuja ili wawe na kuzima, kIsha wawe nao tele” (Yohana 10:10) Jina ‘Yesu’ linamaanisha Mwokozi, Yule atakayetusamehe dhambi zetu.

Neno hili ‘Dhambi’ linamaanisha kuwa katika hali ya kutengwa na Mungu. Asili yetu ilitufanya tutengwe na Mungu nayo matendo yetu hudhihirisha wazi hali hii. Yesu basi alikuja kubadilisha asili yetu na kutufanya wana wa Mungu badala ya wana wa Shetani, Jina Imanueli lilipopewa Yesu lamaanisha Mungu pamoja nasi

Alikuja kama mwanadamu, akanyenyekea na kujiondolea sifa  zote za Mungu na akawa mtu katika hali zote. Alikuja kutukomboa. Jambo hili linafaa kufahamika. Yesu alikuwa zaidi ya mwalimu, alikuwa zaidi ya nabii. Hakika alikuwa Mungu  katika mwili. Mungu pamoja nasi.

Kama tunavyoona akika vitabu vya Injili,Yesu alimdhihirisha Mungu wazi. Alionnyesha upendo, hukumu, haki na huruma za Mungu. Mathayo 8:16-17 husema kuwa Yesu ndiye aliyetimiza ahadi tuliyoangalia katika Isaya 53.

Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo kwa neno lake, akawaponya wote walikuwa hawawezi, ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya akasema, mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukuwa magonjwa yetu. (Mathayo 8:16-17)

Karne nyingi kabla ya Yesu kuja Mungu alitabiri kupitia kwa manabii kuwa Yesu alikuwa akija kufanya kazi hii: kuwakomboa wanadamu kiroho, kimwili na kihisia. Huduma ya uponyaji, ya Yesu indhihirisha kuwa Mungu aliwatembelea watu wake. Anataka kuwapenda watu wakl na kuwakomboa.

## HUDUMA YA YESU

Luka 4:18-19 yatufahamisha zaidi kuhusu huduma ya yesu. Alitimiza yaliyonenwa na nabii Isaya. Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maaana amenitia mafuta kuwahubiria maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru walioteswa na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.

Yesu alikuja akiwa shahidi wa ni nani wa Baba wa mbinguni na atuwezeshaye kupata uzima wa milele. Katika 1 Petro 3 tunayashuhudia mengi aliyoyatenda Yesu.  “Kwa maana Kristo naye mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa hiyo aliiwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiria; watu wasiotii zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenzwa ; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka maji. Mfano wa mambo ambayo ni ubatizo, unawaokoa nyinyi pia siku hizi; (sio kuweka mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu) kwa kufufuka kwake Yesu Kristo. Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake. (1 Petro 3:18-22)

Hii ni kumaanisha kuwa katika jina la Yesu kila goti mbinguni na duniani linapigwa kwa sababu Baba Mungu amedhihirisha Yesu kama Bwana wa wote.

Baada ya kifo chake Yesu alishuka chini na kuwatangazia ushindi wote waliofungwa jela. Aliwahubiria Injili. “Maana kwa ajili hiyo hata hao waliokufa walihubiriwa Injili ili kwamba wahukumiwe katika mwili. Kama wahukumiwavyo wanadamu bali wawe hai katika roho kama Mungu alivyo hai. (1 Petro 4:6)

Injili(habari njema kumhusu yesu) ilihubiriwa waliokuwa wamekufa. Mungu aliwapa fursa wote waliokuwa wamekufa kabla ya Yesu kuja katika ulimwengu kumpokea yeye kama bwana na wawe na uzima wa Mungu kama ulivyodhihirishwa katika Yesu. Kisha Yesu akafufuka kutoka wafu akiwa ametangazwa kuwa Bwana wa yote na mfalme wa wafalme, na katika jina lake kila goti litapigwa.

KUUNGANISHWA KATIKA MPANGO WA MUNGU.

Mungu alikuwa na mpango wetu sisi tulioitwa watu wa mataifa. (Wale ambao hawakuchanguliwa kama Waisraeli), kwa maana Mungu alituunganisha na mzabibu(mpango wake wa uzima). Ametupangia na kututolea uzima sawa na alivyowatolea Waisraeli watu wake wateule. Tunapokea uzima huu kwa kukiri kwa vinywa vyetu Yesu Kristo ni Bwana na jinsi tunavyomhitaji ndani yetu na kuyatawala maisha yetu, ili tumuishie Mungu sasa na sio sisi wenyewe. (Warumi 10:9-10). Mungu ametukarimia hali hii na mpango huo.

Vile vile tunaangalia anacho Mungu kwa Waisraeli, wayahudi. Tunajua kuwa wakati huu wayahudi wengi wamemkataa Bwana. Tunataka kufahamu yanayotendeka na kwa nini yanatendeka.

Tazama Warumi 11:20-24

Vema. Yalikatwa kwa kutokuamini kwao, na wewe wasimama kwa imani yako. Usijivunie bali uogope. Kwa maana ikiwa Mungu hakuyaachia matawi ya asili, wala hatakuachia wewe. Tazama basi, wema na ukali wa Mungu; kwa wale walioanguka, ukali, bali kwako wewe, wema huo; kama sivyo, wewe nawe utakataliwa mbali. Nao hao pia, wasipokaa katika kutoamini kwao, watapandikizwa; kwa kuwa Mungu aweza kupandikiza tena.. kwa maana ikiwa wewe ulikatwa ukatolewa katika mzeituni, ulio mzeituni mwitu kwa asili yake, kisha ukapandikizwa, kinyume cha asili, katika mzeituni ulio mwema, si zaidi sana wale wa asili kuweza kupandikizwa katika mzeituni wao wenyewe? (Alikuwa akinena kuwahusu wayahudi kuingia katika uzima ambao Mungu aliwapangia kutoka mwanzo).

Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msiijue siri hii ili msijione kuwa wenye akili; ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Waisraeli, mpaka utimilifu wa mataifa uwasili. Hivyo Israeli wote wataokoka; kama ilivyoandikwa, mwokozi atakuja kutoka Sayuni: atamtenga Yakobo na

maasia yake. Na hili ndilo agano langu nao, nitakapowaondolea dhambi zao. Basi kwa habari ya Injili wamekuwa adui kwa ajili yenu; bali kwa habari ya kule kuchaguliwa wamekuwa wapenzi kwa ajili ya baba zetu. (Warumi 11:25-28) (Baba zetu ni Ibrahimu, Isaka na Yakobo ambao Mungu aliahidi watakuwa baba wa taifa kubwa na kuwa watu wangebarikiwa)

...Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto wala mwito wake. Kwa maana nyinyi zamani mlivyomuasi Mungu, lakini sasa mmepata rehema kwa kuasi kwao; kadhalika na hao wameasi sasa, ili kupata rehema kwenu nao wapate rehema. (Warumi 11:29-31).

Mungu kwa hekima yake kuu aliifanya mioyo yaWaisraeli migumu ili wasimpokee Yesu, ili sisi tumpokee Yesu na uzima wa Mungu. Huruma za Mungu zitawaondolea hali hii ili nao waweze kupokea uzima ambao Mungu aliwadhamiria kutoka mwanzo katika Yesu Kristo.

Maana Mungu amewafunga wote pamoja katika kuasi ili awarehemu wote. Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani! Maana ni nani aliyejua nia ya Bwana? Au ni nani aliyempa kitu kwanza, naye atalipwa tena? Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake. Utukufu una yeye milele. Amina. (Warumi 32-36)

KURUDI KWA YESU

Tunafahamu pia kuwa Yesu Kristo atarudi tena. Yeye hatakawia. Shetani, malaika walioanguka pamoja na wote wasioamini wataadhibiwa milele. (Tazama ufunuo wa Yohana 20:13, Mathayo 25) Yesu atawachukua wote waliitalo jina lake na kumpokea kama Bwana. Katika jina la Yesu sisi tutakuwa na uzima wa milele pamoja na Mungu.

Wakati unapompokea Yesu katika moyo wako, unaurithi uzima wa Mungu na kuingia katika mpango wake. Kutoka hapo mwanzo Mungu alijua kuwa ataiguza roho yako ukilisikiza neno lake na ukubali, “Bwana nisamehe. Nakuhitaji Yesu. Njoo katika maisha yangu. Njoo katika moyo wangu. Nakukiri ewe Yesu Kristo kama Bwana wangu.”

Mungu alijua kutoka mwanzo kuwa ungeingia katika uzima wake. Alijua kutoka mwanzo kuwa ulihitaji uzima wake. Alijua kuwa ungeupokea uzima huu wakati ulimpokea Yesu.

Yesu anarudi. Yeye atawatupa wote wasioliita jina lake katika ziwa la moto.

Hii sio kusema kuwa Mungu hawapendi wote lakini sio kila mtu aliyeokoka. Kwa nini? Hata ikiwa Mungu hutamani kila mtu aokoke(2 Petro 3:9) si kila mmoja ameamini katika ukweli. Neno la Mungu lasema kuwa watu wamejihukumu wenyewe kwa sababu wamepenhda giza kuliko nuru katika Yesu. (Yohana 3:16-20).

Hivi ndivyo linasema! Tuwe na Yesu mioyoni mwetu ama tukose kuwa naye. Tuokoke au tukose kuokoka. Tuwe na uzima wa Mungu au tukose kuwa nao. Tukiwa na uzima wa Mungu tutamuishia. Yesu alisema, “Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito. (1 Yohana 5:3). Tukitii yale Mungu anatuelekeza kufanya, uzima tele utatujia katika kila hali.

Natushiriki upendo huu wa Mungu na wengine, kwa maana ni kweli. “Mungu wetu atawala! Yesu Kristo ni Bwana!” Ikiwa huna hakika kuwa umo nadani ya mpango wa Mungu tutakuhimiza umwombe na upokee kutoka kwake uzima mpya ambao ameutoa ukiwa tele kwa wote katika Yesu.

SEMA KWA SAUTI,
Baba katika jina la Yesu, nimetambua kuwa maisha yangu yametengwa kutokana nawe. Nisamehe. Nimejua kuwa katika upendo wako ulimtuma Yesu Kristo afe na ukamfufua kutoka wafu ndipo niweze kjupokea mpango wako wa kuzima. Ahsante, Bwana, kwa kunisamehe kwa sababu ya damu ya Yesu. Njoo katika maisha yangu, Yesu. Nakiri kwa kinywa changu kuwa Yesu Kristo ni bwana wangu na najua katika moyo wangu jinsi ulivyofufuka kutoka wafu nami nimefufuka dakika hii kutoka wafu na kuingia uzimani. Ahsante Baba kwa kunipenda na kunifanya mwanao, na kuniwezesha kuingia katika mpango wako wa uzima milele nawe. (Yohana 3:16-18, 1 Yohana 5:9-12, Warumi 10:9-10, 2 Wakorintho 5:17-22)

Ni furaha kiwango gani kitakachokujia wakati parapanda italia na mlio kutoka mbinguni. Utamuona Yesu pamoja na malaika mbinguni wakija kukuchukua uwe naye milele. Utawaona waliokufa wakifufuka kwanza kumpokea Yesu hewani ,ukiajabia yale unayoyaona mara moja mwili wako ambao hufa uutabadilishwa na kuwa mwili wa kiroho ambao hudumu milele. Wewe pia utapanda mbinguni kukutana na Bwana Yesu. (Soma 1 Wathesalonike 4:13-18, 1 Wakorintho 5:42-55 (hasa 51-52), Luka 24:36-43)

Tazama picha hii: Mbingu na dunia zimeondolewa, wanadamu wote wamesimama mbele za Bwana ili wahukumiwe.vitabu vinafunguliwa. Wale wote waliomwamini Yesu na kutii amri zake wanapata majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima. Wao wataokoka. Wale wote waliomkataa Yesu na kuishi katika kuasi watahukumiwa katika kiti cha enzi kikubwa, cheupe na kutupwa kwenye ziwa la moto pamoja na Shetani na malaika walioanguka. (Soma Ufunuo 20:7-15, Mathayo 25:31-46 na 7:21-33)

Hebu fikiria! Mbele za macho yako, Mungu ataumba mbingu mpya na dunia mpya. Kwa sababu ya kuupokea mpango wa Mungu wa uzima kwako, utaiona Yerusalemu mpya ikiteremka kutoka mbinguni kwa Mungu. Nawe utamuona Bwana uso kwa uso milele!. Utukufu kwa Mungu! (Soma Ufunuo 21-22).

© 1985, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™,
all rights reserved, used by permission.
www.glorytogod.org